
# MWELEKEO WA MVUA ZA MSIMU WA MASIKA
# MACHI – MEI, 2024




***Kielelezo 1: Mwelekeo wa mvua za Machi hadi Mei, 2024.***

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

**(IMETHIBITISHWA – ISO 9001:2015, Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga)**

**Dondoo muhimu za msimu wa mvua za Masika; Machi - Mei 2024**

Taarifa hii inatoa uchambuzi wa mwenendo wa mifumo ya hali ya hewa na mwelekeo wa msimu wa mvua za Masika katika kipindi cha Machi – Mei, 2024, ushauri kwa wadau wa sekta na mamlaka mbalimbali kama vile Kilimo na Usalama wa Chakula, Mifugo na Uvuvi, Utalii na Wanyamapori, Uchukuzi, Mamlaka za miji, Nishati, Maji na Madini, Afya pamoja na Menejimenti za Maafa. Baadhi ya mambo muhimu katika taarifa hii ni: -

i. Mvua za Wastani hadi Juu ya Wastani kwa msimu wa Masika, 2024 zinatarajiwa katika maeneo mengi ya nchi yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka.

ii. Ongezeko la mvua linatarajiwa katika kipindi cha mwezi Machi, 2024.

iii. Mvua za Masika zinatarajiwa kuanza wiki ya nne ya mwezi Februari, 2024 katika maeneo mengi na zinatarajiwa kuisha katika wiki ya tatu na ya nne ya mwezi Mei 2024 katika maeneo mengi.

**Athari zinazotarajiwa:**

i. Vipindi vya unyevu wa kuzidi kiasi pamoja na mafuriko vinaweza kujitokeza na kuathiri ukuaji wa mazao na miundombinu ya kilimo.

ii. Kina cha maji katika mito na mabwawa kinatarajiwa kuongezeka.

iii. Magonjwa ya mlipuko yanaweza kujitokeza kutokana na uchafuzi wa maji.

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

**(IMETHIBITISHWA – ISO 9001:2015, Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga)**

## 1. MWENENDO WA MVUA ZA MSIMU (NOVEMBA, 2023 HADI APRILI, 2024) NA MWELEKEO WA MVUA ZA MASIKA (MACHI – MEI), 2024

### *1.1 Mwenendo wa mvua za Msimu (Novemba, 2023 hadi Aprili, 2024)*

Mvua za Msimu zilizoanza mwezi Novemba, 2023 zimenyesha kwa kiwango cha Juu ya Wastani katika mikoa ya Dodoma, Singida, Kigoma, Tabora, Katavi, Iringa, Ruvuma, Lindi, Mtwara na kusini mwa mkoa wa Morogoro na Wastani katika mikoa ya Rukwa, Mbeya, Songwe na Njombe katika kipindi cha Novemba, 2023 hadi Januari, 2024. Mvua hizi zilianza mapema wiki ya kwanza na ya pili mwezi Novemba, 2023 na zilitawaliwa na vipindi vya mvua nyingi zilizochangiwa na uwepo wa El Niño. Katika kipindi kilichosalia cha msimu (Februari hadi Aprili, 2024) mvua zinatarajiwa kuendelea kama ilivyotabiriwa mwezi Oktoba, 2023, ambapo kwa ujumla mvua zilitabiriwa kuwa za Wastani hadi Juu ya Wastani.

### *1.2 Mwelekeo wa mvua za Masika (Machi hadi Mei), 2024*

Msimu wa mvua za Masika ni mahususi kwa maeneo ya nyanda za juu kaskazini mashariki (Mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro), pwani ya kaskazini (kaskazini mwa mkoa wa Morogoro, mikoa ya Pwani (ikijumuisha visiwa vya Mafia), Dar es Salaam, Tanga pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba), ukanda wa Ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Mwanza, Shinyanga, Simiyu na Mara) pamoja na kaskazini mwa mkoa wa Kigoma.

Kutokana na mifumo ya hali ya hewa inayotarajiwa katika kipindi cha Masika (kama inavyoelezwa katika kipengele Na. 2 cha taarifa hii), kwa ujumla mvua za wastani hadi juu ya wastani zinatarajiwa katika maeneo mengi yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka. Ongezeko la mvua linatarajiwa mwezi Machi, 2024 katika maeneo hayo. Maelezo ya kina juu ya mwelekeo wa mvua hizo za msimu ni kama ifuatavyo:

**i. Kanda ya Ziwa Victoria: (Mikoa ya Kagera, Geita, Mwanza, Shinyanga, Simiyu, na Mara) pamoja na kaskazini mwa mkoa wa Kigoma (wilaya za Kakonko na Kibondo):**


Mvua za Masika zinatarajiwa kuwa za Wastani hadi Juu ya Wastani katika maeneo mengi ya ukanda wa Ziwa Victoria pamoja na kaskazini mwa mkoa wa Kigoma. Mvua za nje ya msimu zinazoendelea kunyesha zinatarajiwa kuungana na mvua za Masika 2024. Mvua zinatarajiwa kuisha wiki ya tatu na ya nne ya mwezi Mei, 2024.

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

ii. **Ukanda wa Pwani ya Kaskazini: (kaskazini mwa mkoa wa Morogoro, mkoa wa Pwani (ikijumuisha kisiwa cha Mafia), Dar es Salaam, Tanga pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba):**
Mvua za Wastani hadi Juu ya Wastani zinatarajiwa katika maeneo mengi ya ukanda wa pwani ya kaskazini.

Mvua hizo zinatarajiwa kuanza mapema wiki ya nne ya mwezi Februari, 2024 na kuisha wiki ya tatu na ya nne ya mwezi Mei, 2024.

iii. **Nyanda za Juu Kaskazini Mashariki: (Mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro):**
Mvua katika maeneo haya zinatarajiwa kuwa za Wastani hadi Juu ya Wastani na zinatarajiwa kuanza mapema wiki ya nne ya mwezi Februari, 2024. Mvua hizo zinatarajiwa kuisha wiki ya pili na ya tatu ya mwezi Mei, 2024.




***Kielelezo 2: Kushoto: Mwelekeo wa mvua za Masika (Machi –Mei), 2024 na Kulia: Wastani wa muda mrefu (miaka 30) wa mvua za Masika (1991-2020).***

***Angalizo 1:** Izingatiwe kuwa matukio ya vipindi vya mvua kubwa yanaweza kujitokeza katika Msimu wa Masika, 2024.*

***Angalizo 2:** Mwelekeo wa mvua uliotolewa umezingatia zaidi kipindi cha msimu (miezi mitatu) na hali ya mvua katika maeneo makubwa. Hivyo, viashiria vinavyochangia mwenendo wa mifumo ya mvua na mabadiliko ya muda mfupi katika maeneo madogo utazingatiwa katika uchambuzi wa utabiri wa muda wa kati na mfupi. Watumiaji wa taarifa hii wanashauriwa kufuatilia*

*taarifa za utabiri wa saa 24, siku 10, mwezi na tahadhari kama zinavyotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA).*

## 2. MIFUMO YA HALI YA HEWA

Joto la bahari la juu ya wastani linatarajiwa katika eneo la magharibi mwa Bahari ya Hindi (pwani ya Afrika Mashariki) ikilinganishwa na upande wa mashariki mwa Bahari ya Hindi. Vilevile, joto la bahari la chini kidogo ya wastani linatarajiwa katika eneo la kusini mwa kisiwa cha Madagaska. Hali hii kwa pamoja inatarajiwa kuimarisha mifumo isababishayo mvua nchini kwa kuimarisha kasi na nguvu ya msukumo wa unyevu nyevu kutoka baharini kuelekea katika maeneo ya pwani ya kaskazini na nyanda za juu kaskazini-mashariki. Katika eneo la mashariki mwa bahari ya Atlantiki (pwani ya Angola), joto la bahari la chini kidogo ya wastani linatarajiwa. Hali hii inatarajiwa kuimarisha msukumo wa unyevu nyevu kutoka misitu ya Kongo kuelekea nchini hususan katika maeneo yanayozunguka ziwa Viktoria, kaskazini mwa mkoa wa Kigoma na nyanda za juu kaskazini mashariki. Hata hivyo, hali ya El-Niño inayoendelea katika Bahari ya Pasifiki inatarajiwa kupungua nguvu hususan tunapoelekea mwishoni mwa msimu wa mvua wa MAM, 2024.

## 3. ATHARI NA USHAURI

Athari za kisekta na ushauri uliotolewa hapa chini umeandaliwa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania kwa kushirikiana na wataalam wa sekta husika katika mkutano wa wadau wa hali ya hewa uliofanyika tarehe 19 Februari, 2024. Wadau wa sekta mbalimbali za kiuchumi na kijamii wanashauriwa kupanga na kutekeleza shughuli zao kwa kuzingatia taarifa mahususi za hali ya hewa zinazotolewa na TMA.

### a) Kilimo na Usalama wa Chakula

Vipindi vya unyevu wa kuzidi kiasi pamoja na mafuriko vinaweza kujitokeza na kuathiri ukuaji wa mazao na miundombinu ya kilimo. Magonjwa kama vile ukungu (Fungus) yanatajariwa kuongezeka na kuathiri mazao kama nyanya, ufuta, maharage na mazao jamii ya mizizi. Hata hivyo, shughuli za kilimo zinatarajiwa kuendelea kama ilivyo kawaida katika maeneo mengi.

Wakulima wanashauriwa kuandaa mashamba, kupanda, kupalilia na kutumia pembejeo husika kwa wakati, kutumia mbinu bora na teknolojia za kuzuia maji kutuama shambani, mmomonyoko na upotevu wa rutuba, na kuchagua mbegu na mazao sahihi kwa ajili ya msimu huu wa Masika. Pia, wanashauriwa kuimarisha miundombinu ya kilimo hususan maeneo ya mabondeni pamoja na kudhibiti visumbufu vya mimea ili kupunguza athari zinazoweza kujitokeza. Aidha, wauzaji na wasambazaji wa pembejeo za kilimo wanashauriwa kuhakikisha pembejeo zinapatikana kwa wakati.

### b) Mifugo na Uvuvi

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe: met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

**(IMETHIBITISHWA – ISO 9001:2015, Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga)**

Wafugaji na wavuvi wanatarajiwa kunufaika na upatikanaji wa malisho na chakula cha samaki. Hata hivyo, mlipuko wa magonjwa ya mifugo kama vile ugonjwa wa homa ya bonde la ufa na kuzaliana kwa wadudu wanaosambaza magojwa vinaweza kujitokeza. Vilevile, matukio ya kuongezeka kwa magonjwa ya mwani baharini na kupungua kwa uzalishaji wa mwani kutokana na kupungua kwa kiwango cha chumvi ya maji ya bahari vinatarajiwa.

Wafugaji wanashauriwa kutumia mbinu bora za ufugaji ili kutunza malisho na kuvuna maji ya mvua kwa matumizi ya baadae. Jamii inashauriwa kuweka mipango mizuri ya matumizi bora ya maji na malisho. Wakulima wa mwani wanashauriwa kulima mwani kwenye maji ya kina kirefu ili kuondokana na athari za maji ya mvua yanayokuwa yanaingia baharini. Vilevile, wafugaji na wavuvi wanashauriwa kufuatilia mirejeo ya tabiri za hali ya hewa na ushauri kutoka kwa maafisa ugani ili kupunguza athari zinazoweza kujitokeza na kuongeza tija katika msimu huu wa mvua.

### c) Utalii na Wanyamapori

Hali ya malisho na maji kwa ajili ya wanyamapori katika mbuga na hifadhi inatarajiwa kuwa nzuri. Hata hivyo, mvua za wastani hadi juu ya wastani zinazotarajiwa katika maeneo mengi zinaweza kusababisha kutuama na kusambaa kwa maji na kupelekea kuhama kwa wanyamapori. Hali hii inaweza kupelekea magonjwa ya wanyamapori kusambaa kwa wanyama wanaofugwa na binadamu kutokana na wanyamapori kuingia katika makazi ya jamii zinazozunguka hifadhi na mbuga. Pia, hali hii inaweza kusababisha hatari kwa binadamu na wanyama wanaofugwa kutokana na kushambuliwa na wanyamapori.

Mamlaka husika zinashauriwa kuboresha miundombinu mbalimbali katika hifadhi za wanyamapori na kujenga uelewa kwa jamii ili kupunguza athari zinazoweza kujitokeza. Hivyo basi, jamii inashauriwa kutoa taarifa kwa mamlaka husika endapo wanyamapori wataingia katika makazi ya watu.

### d) Usafiri na Usafirishaji

Kutokana na mvua zinazotarajiwa, sekta ya usafiri na usafirishaji inatarajiwa kuathirika na kupelekea uharibifu wa miundombinu ya barabara na reli, ongezeko la ajali barabarani katika usafiri wa nchi kavu, kuchelewa au kusitishwa kwa safari za nchi kavu, ndege, majini, mawasiliano hafifu angani na kwenye maji na kupelekea kuongezeka kwa gharama za uendeshaji katika usafiri wa anga, nchi kavu na majini. Mamlaka husika na wadau wanashauriwa kuchukua hatua stahiki katika utekelezaji wa matengenezo na ujenzi wa miundombinu mbalimbali pamoja na ukaguzi wa mara kwa mara wa miundombinu ya usafiri na usafirishaji ili kupunguza athari zinazoweza kujitokeza.

### e) Nishati, Maji na Madini

Mvua zinazotarajiwa zitachangia kuongezeka kwa kina cha maji katika mito, maziwa na mabwawa hivyo matumizi sahihi ya maji majumbani na uzalishaji wa umeme ni muhimu

kupewa kipaumbele. Hata hivyo, kupungua kwa ubora wa maji, kuongezeka kwa kifusi cha mchanga maji na uharibifu wa kingo za mito na mtandao wa usambazaji maji pia unatarajiwa.

Sekta ya Madini hususan shughuli za uchimbaji mdogo wa madini, huenda zikaathirika, hivyo tahadhari za kiusalama ni muhimu kuchukuliwa ili kukabiliana na maporomoko ya ardhi na miamba. Mvua zinazotarajiwa huenda zikaathiri mtandao wa usafirishaji na usambazaji wa nishati ya umeme na kupelekea kukosekana kwa umeme. Hivyo, mamlaka husika na wadau zinashauriwa kuzingatia usimamizi endelevu wa rasilimali maji na mgawanyo wake kwa maeneo mbalimbali kama vile shughuli za uchakataji madini, uzalishaji umeme, matumizi ya viwandani na majumbani.

**f) Mamlaka za Miji na Wilaya**

Vipindi vya mvua kubwa vinaweza kusababisha kutuama kwa maji na mafuriko. Hali hii inaweza kusababisha uharibifu wa miundombinu na upotevu wa maisha na mali. Mamlaka za Miji na Kamati za Maafa zinashauriwa kuchukua hatua stahiki ili kukabiliana na athari zinazohusiana na mafuriko ikiwa ni pamoja na shughuli za utafutaji, uokoaji na msaada wa kitabibu.

**g) Sekta ya Afya**

Magonjwa ya mlipuko yanaweza kujitokeza kutokana na uharibifu wa miundombinu ya maji unaoweza kusababishwa na maji ya mvua kutuama na kutiririka. Mamlaka za Afya na jamii zinashauriwa kuchukua tahadhari stahiki ili kupunguza athari za kiafya zinazotarajiwa kwa kuharibu mazalia ya mbu, kutibu maji kabla ya kuyatumia, kunywa maji safi na salama pamoja na kuhakikisha uwepo wa dawa na vifaa tiba vya kutosha katika vituo vya Afya.

**h) Sekta Binafsi**

Sekta binafsi inatarajiwa kunufaika na mvua zinazotarajiwa katika msimu huu wa Masika hususan katika shughuli za kilimo, uzalishaji viwandani, n.k. Hata hivyo, wingi wa mvua unaweza kupelekea athari katika shughuli za ujenzi wa miundombinu, uhifadhi na usafirishaji wa mazao tete na bidhaa.

Sekta binafsi zinashauriwa kushirikiana na wataalam mbalimbali ikiwemo wataalam wa hali ya hewa ili kukabiliana na athari zinazoweza kujitokeza. Taasisi mbalimbali zikiwemo Benki na Bima zinashauriwa kuandaa na kutoa huduma mahususi kwa wadau ili kujenga ustahamilivu katika biashara.

**i) Menejimenti za Maafa**

Vipindi vya mvua kubwa vinaweza kujitokeza na kusababisha mafuriko na maporomoko ya ardhi na kupelekea uharibifu wa miundombinu, mazingira, upotevu wa mali na maisha. Hivyo,

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

mamlaka husika katika idara mbalimbali na idara ya Menejimenti ya Maafa nchini zinashauriwa kuendelea kuratibu utekelezaji wa mipango itakayosaidia kupunguza madhara yanayoweza kujitokeza. Aidha, sekta, mamlaka husika na Kamati za Usimamizi wa Maafa katika ngazi ya Mkoa, Wilaya, Kata na Vijiji/Mitaa zinashauriwa kushirikiana na kuchukua hatua stahiki ikiwemo kutoa elimu na miongozo itakayohamasisha kuzuia au kupunguza madhara, kujiandaa, kukabiliana na maafa na kurejesha hali endapo maafa yatatokea.

**j) Vyombo vya Habari**

Vyombo vya Habari vinashauriwa kupata, kufuatilia na kusambaza taarifa za utabiri na tahadhari, pindi tu zinapotoka ili jamii iweze kuzipata kwa wakati. Vilevile, vinashauriwa kutafuta ushauri wa kitaalamu kutoka katika sekta husika wakati wa kuandaa, kutayarisha na kusambaza taarifa za hali ya hewa kwa watumiaji. Pia, inapendekezwa kutumia lugha nyepesi wakati wa kuhabarisha jamii.

*Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania inawashauri watumiaji wote wa taarifa za hali ya hewa ikiwa ni pamoja na wakulima, wafugaji, mamlaka za wanyamapori, wasafirishaji, mamlaka za maji, afya, shughuli za ujenzi (Makandarasi), uchimbaji madini, upakuaji na ushushaji mizigo Bandarini kuendelea kutafuta, kupata na kuzingatia ushauri wa wataalam katika sekta husika.*

*Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania itaendelea kufuatilia mwenendo wa mifumo ya hali ya hewa na kutoa mirejesho ya mwelekeo wa mvua na hali ya hewa kwa ujumla nchini kadri inavyohitajika. Aidha, wadau wanashauriwa kuwasiliana na Mamlaka ili kupata taarifa mahsusi za mwelekeo na utabiri wa hali ya hewa ili kukidhi mahitaji maalum katika sekta zao.*

***Imetolewa: Tarehe 22 Februari, 2024.***
***Na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania:***

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

**(IMETHIBITISHWA – ISO 9001:2015, Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga)**